**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG'**

**SHULE YA SEKONDARI LALAJI**

**S. L. P 198,**

**KATESH – MANYARA**

**Simu: 0768 493 472/0683 866 448**

**02/12/2022**

Kumb.Na. LLSS/ ADMIN/ VOL 01/K1. 2023

MZAZI/ MLEZI WA MWANAFUNZI ……………………………………………………

SHULE YA MSINGI ……………………………………

S. L. P ……………………………...

KATESH – HANANG'

YAH**: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LALAJI WILAYA YA HANANG' MKOA WA MANYARA, KIDATO CHA KWANZA, 2023**

## 1.0 UTANGULIZI

Ninayofuraha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari LALAJI kidato cha kwanza mwaka 2023**. Hongera sana**. Aidha kwaniaba ya Bodi ya shule, walimu na wafanyakazi wa Shule ya Sekondari Lalaji ninakukaribisha**"karibuni sana shule ya Sekondari Lalaji".**

## 1.1 MAHALI SHULE ILIPO

Shule ya Sekondari Lalaji ipo katika kijiji cha Lalaji , kata ya Lalaji, Tarafa ya Balangdalalu, Wilaya ya Hanang' katika mkoa wa Manyara. Shule iko kilometa 1.8 kutaka makao makuu ya kata ya Lalaji na barabara ya kutoka balang'dalalu kwenda Murumba.

## 1:2 TAREHE YA KURIPOTI

Mhula wa masomo kwa mwaka 2023 unaanza **tarehe 09/01/2023**. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **09/01/2023** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **22/01/2023**

Ufikapo shuleni fika ofisi ya makamu mkuu wa shule kwaajili ya usajili. **Hairuhusiwi kuingia darasani kabla ya kusajiliwa**.

## 1:3 AINA YA SHULE

Shule hii ni ya kutwa kwa wanafunzi wote wavulana na wasichana kidato cha kwanza hadi cha nne.

Mawasiliano hapa shuleni ni kwa lugha ya kiingereza.

## 1:4 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 1.1 Sare za shule

**Sare za shule na rangi zake**

**i. Wavulana**

1. Suruali mbili Rangi ya kijani kibichi**(angalia rangi ya kitambaa kilicho ambatishwa na fomu hii)**zenye mfuko mmoja wenye kuingia ndani, looks 8 yaani mbele nne (kushoto mbili na kulia mbili), nyuma mbili na pembeni mbili. Vili vile iwe na marinda manne( 4 celebrations) mawili kila upande. Hakikisha sare ni mpya na isiwe ya kubana upana chini kuanzia inch 15.
2. Unatakiwa kuwa na mashati mawili meupe mikono mifupi aina ya tetroni yenye mfuko mmoja na yasiwe ya cotton (pamba)
3. Sweta 1 au 2 zenye rangi inayofanana na suruali, sweta liwe na**"V"**
4. Soksi jozi mbili za rangi nyeusi
5. Mkanda wa suruali ambao ni mweusi wangozi (usiwe na mapambo).
6. Tai inayofanana Rangi na kitambaa cha suruali.
7. Tracksuit moja rangi ya dark blue kwaajili ya michezo, ni muhimu sana. ***** suruali inayobana,mnyonyo na mlegezo haviruhusiwi *****

**ii. Wasichana**

1. Sketi mbili Rangi ya kijani kibichi (**angalia rangi ya kitambaa kilicho ambatishwa na fomu hii**) ziwe ndefu hadi kwenye vifundo vya miguu, marinda 16, belt inchi mbili na pindo la nchi moja.
2. Blauzi mbili nyeupe za mikono mifupi aina ya tetroni, ziwe na mfuko mmoja tu na zisiwe za cotton (pamba).
3. Sweta moja au mbili za uzi unaofanana na sketi, sweta liwe na "**V"**
4. **Tai inayofanana Rangi na kitambaa cha sketi.**
5. Soksi jozi mbili ndefu za rangi nyeupe
6. Kwa waislamu juba/ushungi uwe warangi nyeupe, juba/ushungi iwe usawa wa kifua na sketi zao ziwe ndefu hadi vifundo vya miguu. Ushungi usiwe na urembo, kitambaa cha juba/ ushungi visiwe vyenye kuangaza (transparent). Blauzi nyeupe na yenye mikono mirefu. **SURUALI HAIRUHUSIWI**
7. Tracksuit moja rangi ya dark blue kwaajili ya michezo, ni muhimu sana.

Unatakiwa kuwa na jozi mbili za viatu vya ngozi vyenye rangi nyeusi na vyenye kufunga na Kamba (gidamu) visivyo na visigino virefu. Viatu maarufu kwa jina la bajaji ,raba na aina nyingine kama hiyo hiviruhusiwi shuleni.

**NB: uvaaji wa sare za shule ni muhimu na ni lazima uwe na sare ya shule yenye heshima na itakaguliwa ukifika shuleni kama tulivyo kuagiza katika fomu hii.**

1.2 **Mahitaji Binafsi ya Mwanafunzi/ vitendea kazi darasani na usafi wa mazingira**.

I. Madaftari makubwa 09 (counter book quire 3) ya kuandikia notes
II. Madaftari madogo 09 yenye kurasa 48 au 96 ya kufanyia mazoezi
III. Jalada (spring file) la kutunzia mitihani unayoifanya
IV. Kalamu za kutosha, penseli, rula, kifutio cha penseli na mkebe wa vifaa vya mahesabu (mathematical set), kamusi ya kiingereza(english to english dictionary )

V. Rim moja yenye mistari kwaajili ya majaribio mbalimbali ya wiki na mwezi ilikuepuka kuchana karatasi kwenye madaftari.
VI. Ufagio/chelewa kwaajili ya usafi wa darasa na mazingira ya shule
VII. Jembe moja lenye mpini kwa wavulana.
VIII. Kwanja kwa wasichana

NB.Gharama za Matibabu kwa mwanafunzi ni jukumu la mzazi mwenyewe

**1.3 Chakula cha wanafunzi na mahitaji yake**

Ni jukumu la mzazi kuleta chakula cha mtoto wako awapo shuleni na jamii kwa ujumla.Chakula shuleni kinaratibiwa na kamati ya chakula ya wazazi.

- Mahitaji ya wanafunzi wa kutwa
  - Mahindi debe 4 kwa mwaka au debe 2 kwa mhula
  - Maharage debe 2 kwa mwaka au debe 1 kwa mhula
  - Fedha kwaajili ya posho ya mpishi, sukari, mafuta, chumvi, maji, kuni kusaga n.k ni Tshs. 60,000/= kwamwaka au 30,000/= kwa mhula
  - Sahani na kijiko kwaajili ya chakula.

**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

1.4 Mambo ya kuzingatia

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sharia namba 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewanaWizara ya Elimu Sayansi naTeknolojia, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na uendeshaji Elimu. Kama mwanafunzi unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa vizuri mara baada ya kuripoti shuleni:

I. Heshima kwa Viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
II. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani ya shule kulingana na ratiba ya shuleni lazima;
III. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio baada ya vipindi vya darasani (preparatrion)
IV. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
V. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na n je ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
VI. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
VII. Kuvaa sare ya shule kikamilifu wakati wote unapotakiwa;
VIII. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
IX. Kutunza mali za shule Umma na mali binafsi.
X. Ni lazima mwanafunzi ahudhurie shule siku zote 195 kwa mwaka na kwa masomo yote kwa siku. **UTORO** wa shule/ vipindini **MWIKO**. Mzazi kama kuna shida tafadhali toa taarifa shuleni.

**1.6 Makosa yanayoweza kusababisha kusimamishwa au kufukuzwa shule**

I. Wizi
II. Uasherati na ushoga
III. Ubakaji
IV. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadhalika.
V. Kupigana au kupiga

VI. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
VII. Kudharau bendera ya Taifa
VIII. Kuwa mjamzito, kupata mimba au kusababisha mimba
IX. Kutoa mimba
X. Kuoa au kuolewa
XI. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu
XII. Kukataa adhabu kwa makusudi
XIII. Kuwa na simu ya mkononi.

**2.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

2.1 **Fomu ya daktari: Medical Examination Form** ambayo itajazwana Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni. Fomu imeambatanishwa.

**HITIMISHO:**Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

***TAKUTAKIA MAANDALIZI MAZURI KARIBU SANA***

**…………………………………………**

**KENEDY M.MBILINYI**

**MKUU WA SHULE LALAJI SEKONDARI**

Kiambatisho N0. 1

**CERTIFICATE OF MEDICAL EXAMINATION**

LALAJI SECONDARY SCHOOL,
P.O BOX 198
KATESH – MANYARA
Date ……………………………………….

Ref No. HSS/HCU/HD/22
The Medical Officer,
Government Hospital/DDH …………………………………….
P.O Box ………………………………….

Dear Doctor

**RE: SPECIAL REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

NAME OF PUPIL ……………………………………………………… FORM I YEAR 2022

We shall be grateful if you will kindly examine the above-named pupil and give us a report to undertake in our school well. Please remark and indicate against the item mentioned below:

I. X- Ray ………………………………………………………………
II. Urine …………………………………………………………...
III. Stool examination ………………………………………………...
IV. Physical fitness ... Eyes, limbs, Chest, Ears, Spleen, Abdomen, Speech …………………
V. V. D ………………………………………………………………
VI. Tuberculosis (T. B) ……………………………………………………
VII. Pregnancy test ……………………………………

A. **PRELIMINARY INFORMATION FROM THE PUPIL BEFORE THE DOCTOR**

Historical Background

| S/N | DISEASE | YES/NO | S/N | DISEASE | YES/NO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Tuberculosis | | 10 | Epilepsy | |
| 2 | Asthma | | 11 | ENT Trouble | |
| 3 | Pneumonia | | 12 | Skin disorder disease | |
| 4 | Heart trouble | | 13 | Anemia | |
| 5 | Recurrent indigestion | | 14 | Operations | |
| 6 | Jaundice | | 15 | Serious accidents | |
| 7 | Dysentery | | 16 | Chronic Malaria | |
| 8 | Kidney & urine trouble | | 17 | Stomach trouble | |
| 9 | Nervous break down | | 18 | Eye disorder | |

**OFFICIAL MEDICAL EXAMINATION REPORT**

Weight………………. Heart Beat ……………... vision ……………...E.CT …………………………….

Doctor’ s Name …………………………… Designation ……………………. Date …………………...

Signature and Official Stamp, ………………………………………………….